SUMBAWANGA CATHOLIC DIOCESE
PREVENT and CURE
Diocesan Health Board

Namanyere DDH P.O.BOX 17 Namanyere Nkasi Rukwa Tanzania
E,A Fax 025 -2830127 Tel 025 -283002
Email namanyereddh@yahoo.com

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.

Ofisi ya Mganga Mkuu Hospitali Teule ya Namanyere (NDDH) imepata kibali cha Ajira Mpya saba (7) kwa barua ya Katibu Mkuu Kumb. **Na. FA.10/128/01"L"/53** ya tarehe **14 Septemba, 2022** kwenye Ikama ya mwaka 2022/2023. Hivyo Mganga Mkuu Namanyere (NDDH) anakaribisha maombi ya kazi kwa watanzania wenye sifa zifuatazo:-

**1.0. Daktari (wa Binadamu) II -TGHS E1. (Nafasi 1 )**

**1.1. Sifa za mwombaji:**

Sifa za kuingia moja kwa moja Kuajiriwa wenye Shahada ya Udaktari kutoka Vyuo Vikuu/Vyuo vinavyotambuliwa na Serikali waliomaliza "Internship" na kupata usajili kutoka Baraza la Madaktari Tanganyika (Medical Council of Tanganyika).

**1.2. Kazi na majukumu:**

- Kufanya kazi zote za matibabu Hospitalini zinazohusiana na magonjwa mbalimbali yakiwemo magonjwa ya watoto, magonjwa ya akina mama na upasuaji wa kawaida na wa dharura.
- Kutoa na kusimamia elimu ya afya pamoja na kuboresha afya ya jamii katika Wilaya na Mikoa au eneo lake la kazi.
- Kuchunguza, kufuatilia na kuzuia milipuko ya magonjwa
- Kutunza takwimu na kuzitumia kama inavyoelekezwa katika misingi ya MTUHA.
- Kupanga na kutathimini huduma za afya katika eneo lake la kazi.
- Kufundisha wanafunzi na watumishi waliopo kwenye eneo la kazi
- Kusimamia na kuelekeza wafanyakazi walio chini yake
- Kufundisha wanafunzi katika vyuo vya afya vilivyopo eneo lake la kazi
- Kubuni na kuendesha utafiti na kusambaza matokeo
- Kubuni na kutayarisha mikakati ya kuinua ubora wa huduma ya fani yake

**1.3. Mshahara.**

- Atalipwa mshahara kwa viwango vilivyopo vya serikali kulingana na miundo ya sekta ya Afya yaani TGHS E1.

**2.0 Muuguzi. II- TGHS A1 (Nafasi 3).**

**2.1. Sifa za mwombaji:**

Sifa za kuajiriwa moja kwa moja Kuajiriwa wenye cheti cha Uuguzi cha miaka miwili kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali na kuandikishwa (Enrolled) na Baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania.

CS CamScanner

### 2.2. Kazi na majukumu.

- Kufanya kazi za kiuguzi za kuhudumia wateja katika jamii, hospitali na sehemu zote zinapotolewa huduma za afya.
- Kusimamia na kuratibu kazi zote za wahudumu wa afya katika sehemu yake ya kazi
- Kukusanya takwimu na kutayarisha taarifa za utendaji wake wa kazi
- Kutoa huduma kwa wagonjwa majumbani.
- Kutoa ushauri nasaha
- Kutoa huduma za kinga na uzazi wa mpango
- Kutoa huduma za uzazi na afya ya mtoto
- Kuelimisha wagonjwa na jamii kuhusu matatizo yao ya kiafya
- Kufuatilia utunzaji wa vitendea kazi katika maeneo yake ya kazi
- Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

### 2.3. Mshahara.

- Atalipwa mshahara kwa viwango vilivyopo vya serikali kulingana na miundo ya sekta ya Afya yaani TGHS A1.

## 1.0. Afisa Muuguzi Msaidizi II – TGHS B1 (Nafasi 1)

### 1.1. Sifa za Mwombaji

Kuajiriwa wenye Stashahada (Diploma) ya Uuguzi, kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali, waliosajiliwa na Baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania.

### 1.2. kazi na majukumu.

- Kutoa huduma za uuguzi
- Kukusanya takwimu muhimu za afya.
- uwaelekeza kazi wauguzi walio chini yake
- Kuelimisha wagonjwa na jamii kuhusu matatizo yao ya kiafya
- Kutoa huduma za kinga na uzazi
- Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake

### 1.3. Mshahara.

Atalipwa mshahara kwa viwango vilivyopo vya serikali kulingana na miundo ya sekta ya Afya yaani TGHS B1.

## 2.0. Afisa Sayansi Maabara Ya Afya II (RADIOLOGY) – TGHS C1 (Nafasi 1)

### 2.1. Sifa za mwombaji

CamScanner

Kuajiriwa wenye Shahada ya Sayansi katika fani ya Radiolojia kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali na kusajiliwa na Mabaraza ya Taaluma pale inapohusika.

**2.2. Kazi na majukumu.**

- Kufanya vipimo vya aina mbalimbali vya radiolojia.
- Kutunza mitambo na vifaa vya Radiolojia katika eneo lake la kazi
- Kuhakikisha ubora wa picha za X-Ray
- Kutunza picha za wagonjwa hadi majibu yanapowafikia madaktari waliowatuma wagonjwa 72
- Kusimamia watumishi walio chini yake
- Kuandaa vifaa vya tiba/uchunguzi na kusimamia utakasaji vifaa
- katika eneo lake la kazi (sterilization)
- Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi
- zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake

**2.3. Mshahara.**

- Atalipwa mshahara kwa viwango vilivyopo vya serikali kulingana na miundo ya sekta ya Afya yaani TGHS C

**3.0. Tabibu II -TGHS B1 ( Nafasi 1)**

**3.1. Sifa za mwombaji**

- Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha nne/sita wenye Stashahada ya Tabibu/Tabibu Meno kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali.

**3.2. Kazi na majukumu**

- Kazi zote zinazofanywa na Tabibu Msaidizi
- Kutambua na kutibu magonjwa ya kawaida
- Kusimamia utendaji wa watumishi walio chini yake na kufanya upasuaji mdogo
- Kushiriki katika kupanga na kutekeleza Huduma za Afya Msingi
- Kushauri na kuhamasisha wananchi kuchangia huduma za Afya za Mfuko wa Afya ya Jamii
- Kuweka kumbukumbu za vifaa na zana za kutolea huduma
- Kuweka kumbukumbu, kuandaa na kutoa taarifa za utekelezaji
- Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi

**3.3. Mshahara.**

- Atalipwa mshahara kwa viwango vilivyopo vya serikali kulingana na miundo ya sekta ya Afya yaani TGHS B1.

CamScanner

**MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE.**

- Waombaji wote wawe Raia wa Tanzania wenye umri wa kati ya miaka 18-45.
- Maombi yote yaambatishwe na cheti cha kuzaliwa pamoja na nakala za vyeti vya shule na vya taaluma husika.
- Maombi yote yaambatishwe maelezo binafsi (CV) ya mwombaji husika yenye anwani na namba za simu pamoja na majina ya wadhamini watatu na namba zao za simu.
- Maombi yote yaambatishwe na picha moja ya passportsize iliyopigwa hivi karibuni.
- Testimonials, provisional Results, statement of Results, Hati za matokeo ya kidato cha IV na VI (yaani form IV and VI Result slips) havitakubaliwa.
- Hatua kali za kisheria na kiutawala zitachukuliwa kwa watakaoghushi vyeti katika maombi haya.
- Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 03/11/2022 saa **8:00** mchana. Aidha, Halmashauri ambayo ni www.nkasidc.go.tz, na Website ya sekretarieti ya Ajira www.ajira.go.tz na kwenye mbao za matangazo.
- Maombi yanaweza kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili fasaha au Kiingereza fasaha na yatumwe kwa posta kwa anwani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji (W),
S.L.P 02,
**NAMANYERE – NKASI.**

NAMANYERE DESIGNATED DISTRICT HOSPITAL
MEDICAL OFFICER IN CHARGE
DATE.......

...............................
PD. COSMAS MAKASI
KNY: MGANGA MFAWIDHI
**HOSPITALI TEULE YA NAMANYERE**

**NAKALA:**

- Katibu Tawala (M)
  S.L.P 128,
  **SUMBAWANGA.**

- Katibu Tawala(W)
  S.L.P 1,
  **NKASI.**

- Mbao zote za matangazo
  Halmashauri ya Wilaya,
  **NKASI.**

CamScanner